JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

Telegrams: "UTUMISHI", DAR ES SALAAM
Tel. No. : +(255) 22 2118531-4
Fax No.: +(255) 22 2125299
E-mail: permsec@utumishi.go.tz

OFISI YA RAIS
MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA
UTUMISHI HOUSE
8 BARABARA YA KIVUKONI
S.L.P 2483
11404 DAR ES SALAAM

Unapojibu tafadhali taja:

Kumb. Na.EG.45/86/01 `D'/1

24 Februari, 2015

YAH: WARAKA WA UTUMISHI NA.1 WA MWAKA 2015 KUHUSU UTEKELEZAJI WA MWONGOZO WA UFUATILIAJI WA UZINGATIAJI WA MAADILI KATIKA UTUMISHI WA UMMA

1.0 Utangulizi

1.1 Mwaka 1998, Serikali iliandaa na kutoa Kanuni za Maadili ya Utendaji katika Utumishi wa Umma. Kanuni hizi zilihuishwa mwaka 2005 ili kuzifanya ziendane na wakati. Aidha, Ofisi hii imekuwa ikitoa machapisho ya magazeti na vipindi mbalimbali vya Redio na Televisheni kwa lengo la kuelimisha na kuhamasisha uzingatiaji wa maadili katika Utumishi wa Umma.

1.2 Sambamba na Kanuni hizo, Taasisi za Umma nazo zimekuwa zikichukua hatua mbalimbali kwa lengo la kuimarisha uadilifu wa watumishi wa taasisi hizo. Juhudi hizo ni pamoja na kutoa mafunzo ya Maadili, Sheria, Kanuni na Taratibu, kuimarisha mifumo ya ufuatiliaji, kuboresha mazingira ya kazi, kuendeleza watumishi na kuchukua hatua dhidi ya watumishi wanaokiuka Maadili, Sheria, Kanuni na Taratibu.

1.3 Kufuatia hatua hizi za kuimarisha maadili katika utumishi wa umma, Serikali imekuwa ikifanya tafiti mbalimbali kupima kiwango cha uzingatiaji maadili katika utumishi wa umma ili kuona kuwa kanuni hizo zinazingatiwa, na kama sivyo, iweze kuchukuwa hatua za kuimarisha zaidi.

2.0 Tathmini za uzingatiaji Maadili katika Utumishi wa Umma

2.1 Tathmini ya kwanza ilifanyika kupitia utafiti uliofanyika mwaka 2006 (Ethics Baseline Opinion Survey), kwa lengo la kuandaa viwango (baseline) ambavyo vingetumika kama msingi wa kupima maendeleo ya ukuaji wa maadili mema katika Utumishi wa Umma. Utafiti huo ulionesha kuwa kwa kuzingatia kipimo maalum cha uzingatiaji maadili (Ethical Conduct Index), kiwango cha uzingatiaji maadili katika utumishi wa umma kilikuwa ni asilimia 56.9 kutokana na maoni ya wadau waliohojiwa.

2.2 Kufuatia hatua zilizoelezwa katika aya ya 1 ya Waraka huu, Serikali ilifanya tathmini nyingine mwaka 2014 (Tanzania Public Service Integrity Survey), kwa lengo la kupima maendeleo ya kuongezeka kwa kiwango cha uzingatiaji wa maadili miongoni mwa watumishi wa umma. Utafiti huo ulibainisha kuwa kiwango hicho kilifika asilimia 66.1 mwaka 2014.

2.3 Pamoja na kiwango cha uzingatiaji wa maaadili kuongezeka, utafiti huo ulionesha kuwa pamoja na mambo mengine, hakuna mfumo mahsusi wa ufuatiliaji uzingatiaji wa Maadili katika Utumishi wa Umma. Kukosekana kwa mfumo huo kumesababisha kuendelea kuwepo udhaifu katika usimamizi wa uzingatiaji wa Maadili. Kutokana na hali hiyo, Serikali imeandaa Mwongozo wa namna Taasisi za Umma zitakavyofanya ufuatiliaji na tathmini za mara kwa mara kupima kiwango cha uzingatiaji maadili ili kuwa na utumishi wa umma uliotukuka kimaadili.

3.0 Madhumuni ya Waraka huu

Madhumuni ya Waraka huu ni kuwataka Waajiri wote katika Utumishi wa Umma kutekeleza ipasavyo Mfumo wa Ufuatiliaji wa Uzingatiaji Maadili ya Utumishi wa Umma katika utekelezaji wa shughuli za umma.

4.0 Maeneo ya kuzingatiwa katika Ufuatiliaji wa Uzingatiaji Maadili

4.1 Ufuatiliaji na tathmini ya uzingatiaji wa maadili uliofafanuliwa katika Mwongozo huu utakuwa katika maeneo makuu mawili ambayo ni kuwapima watumishi wanavyozingatia Kanuni za

Maadili ya Utendaji katika Utumishi wa Umma na jinsi Taasisi za Umma zinavyoweka mazingira au kuimarisha miundombinu ya maadili inayochangia kuwepo kwa uadilifu miongoni mwa watumishi wake. Maelekezo ya kina yametolewa katika Kijitabu cha **MWONGOZO WA UFUATILIAJI WA UZINGATIAJI WA MAADILI KATIKA UTUMISHI WA UMMA CHA MWAKA 2014.**

4.2 Ili kuhakikisha kuwa Mwongozo huu unatekelezwa ipasavyo Mamlaka zote za Ajira zinawajibika kutekeleza yafuatayo:-

(i) Kufanya suala la uzingatiaji wa maadili kwa Watumishi wa Umma kuwa ni suala muhimu linalofuatiliwa, kujadiliwa na kutolewa taarifa mara kwa mara;

(ii) Kuusoma na kuuelewa vizuri Mwongozo wa Ufuatiliaji wa Uzingatiaji wa Maadili katika Utumishi wa Umma na kuutekeleza ipasavyo;

(iii) Kuhakikisha kuwa Kanuni za Maadili ya Utendaji katika Utumishi wa Umma na miongozo mingine ya Maadili inapatikana kwa watumishi kwa kuwagawia nakala, kuweka kwenye Tovuti na kuweka kwenye sehemu ya wazi kama vile Maktaba au "Resource Center";

(iv) Kuhakikisha kuwa mafunzo ya Maadili yanatolewa kwa watumishi wa Taasisi kila mwaka ili kuwaelewesha, kuwahamasisha na kuwakumbusha wajibu wao wa kuzingatia maadili;

(v) Kuhakikisha kuwa watumishi katika Taasisi wanazingatia Kanuni za Maadili ya Utendaji katika Utumishi wa Umma kwa kuwa na utaratibu wa kufanya ufuatiliaji wa mara kwa mara ili kubaini iwapo watumishi wanazingatia maadili;

(vi) Kuteua Afisa au Maafisa Mahsusi watakaofuatilia na kuratibu uzingatiaji wa maadili kwenye Taasisi;

(vii) Kuunda Kamati ya Uadilifu na kuhakikisha kuwa inafanya kazi;

(viii) Kuwachukulia hatua watumishi wanaokiuka Kanuni hizo kwa mujibu wa Sheria, Kanuni na Taratibu za uendeshaji wa masuala ya nidhamu katika Utumishi wa Umma;

(ix) Kuandaa na kutoa taarifa zinazohusu matokeo ya Ufuatiliaji na Tathmini zinazofanyika mara kwa mara na zinazofanyika katika vipindi mahsusi kuhusu uzingatiaji wa Maadili kwa Mamlaka mbalimbali za Serikali na Wadau, na

(x) Kusimamia watumishi kutoa Ahadi za Uadilifu (Integrity Pledges) kama njia mojawapo ya kuonesha uwajibikaji wao katika suala la uzingatiaji wa maadili.

4.3 Utekelezaji wa Mwongozo huu utasaidia Watumishi wa Umma kujirekebisha au kuwa na tabia na mienendo stahiki wanapokuwa kazini na hivyo kuongeza ari ya kufanya kazi, kuboresha utoaji wa huduma kwa Umma, kuongeza tija na kuokoa rasilimali za umma zinazopotea kwa ukosefu wa maadili.

5.0 Utekelezaji wa Waraka huu

Waraka huu unawahusu watumishi wote wa Umma na unaanza kutumika kuanzia tarehe **1 Machi, 2015.**

George D. Yambesi
KATIBU MKUU (UTUMISHI)